TANGAZO LA SERIKALI NA. 25 la Tarehe 17/02/2017

SHERIA YA FEDHA YA SERIKALI ZA MITAA

(SURA YA 290)

# SHERIA NDOGO

*Zimetungwa chini ya kifungu cha 7(1) na 16(1)*

SHERIA NDOGO (ADA NA USHURU) ZA HALMASHAURI YA WILAYA YA MLELE ZA MWAKA 2017

## SEHEMU YA KWANZA

## UTANGULIZI

Jina na tarehe ya kuanza kutumika

1. Sheria Ndogo hizi zitajulikana kama Sheria Ndogo za (Ada na Ushuru) za Halmashauri ya Wilaya ya Mlele za Mwaka 2017 na zitaanza kutumika baada ya kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali.

Matumizi

2. Sheria Ndogo hizi zitatumika katika eneo lote lililo chini ya mamlaka ya Halmashauri ya Wilaya ya Mlele

Tafsiri

3. Katika Sheria Ndogo hizi isipokua pale itakapoelezwa vinginevyo:-

"Ada na Ushuru" maana yake ni malipo yanayolipwa kwa Halmashauri au wakala wake kwa ajili ya huduma, vibali, au leseni mbalimbali zitolewazo na Halmashauri;

"Afisa Mwidhiniwa" maana yake ni Afisa yeyote wa Halmashauri aliyeteuliwa kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hizi;

*Tangazo la Serikali Na. 25 (Linaendelea)*

"Chombo cha Usafiri" maana yake ni chombo chochote kinachotumika kusafirisha mtu, watu au mizigo kutoka sehemu moja kwenda nyingine isipokuwa mkokoteni, au wanyama wanaotumika kama kusafirisha watu au mizigo;

"Halmashauri" maana yake ni Halmashauri ya Wilaya ya Mlele;

"Kibali" maana yake ni idhini au ruhusa ya maandishi inayotolewa na Halmashauri;

"Machinjio" maana yake ni sehemu iliyotengwa na Halmashauri kwa ajili ya kuchinjia wanyama na kuanika ngozi;

"Masoko" maana yake ni sehemu yoyote iliyotengwa na Halmashauri kwa ajili ya kuuza na kununua bidhaa;

"Mnada" maana yake ni sehemu iliyotengwa na Halmashauri kwa ajili ya kuendesha shughuli za kuuza na kununua bidhaa;

"Mkurugenzi" maana yake ni Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Mlele pamoja na Afisa yeyote wa umma atakayeteuliwa kutekeleza majukumu ya Mkurugenzi.

"Usajili wa vyombo vya usafiri" maana yake ni utaratibu utakaowekwa na Halmashauri wa kuorodhesha idadi ya vyombo vya usafiri vinavyofanya biashara ndani ya mamlaka ya halmashauri;

vibao vya matangazo maana yake ni ubao, ukuta au mahali popote au chombo chochote ambacho kimewekewa tangazo la biashara

"Wakala" maana yake ni Mtu, Taasisi, Kampuni, au asasi yeyote iliyoteuliwa kisheria na Halmashauri kukusanya mapato kwa niaba ya halmashauri.

*Tangazo la Serikali Na. 25 (Linaendelea)*

## SEHEMU YA PILI
## NAMNA YA KUKUSANYA ADA NA USHURU

Ada na Ushuru

4. -(1) Halmashauri itatoza Ada na Ushuru mbalimbali kwa ajili ya vibali, leseni na huduma zitolewazo na Halmashauri kama inavyoonyeshwa katika Jedwali la Kwanza la Sheria Ndogo hizi.

(2) Ada na Ushuru utozwayo chini ya Sheria Ndogo hizi utalipwa kabla ya huduma kutolewa.

(3) Huduma zitakazotozwa Ada na ushuru katika Sheria Ndogo hizi ni;-

(a) Ushuru wa Mazao;

(b) Ushuru wa mifugo na machinjio;

(c) Ushuru wa soko;

(d) Ada ya kibali cha kufanya biashara zisizohitaji leseni;

(e) Ada ya kibali cha ujenzi;

(f) Ada ya Ukaguzi wa ramani;

(g) Ada ya kuchangia gharama za upimaji na usafishaji wa viwanja;

(h) Kodi ya ardhi (Land rent);

(i) Ada ya Leseni mbalimbali;

(j) Ada ya Zabuni;

(k) Ada ya Uthamini wa ardhi;

*Tangazo la Serikali Na. 25 (Linaendelea)*

(l) Ada ya kibali cha kusafirisha ngozi;

(m) Ada ya kukodi mali za Halmashauri;

(n) Faini ya adhabu kwa makosa mbalimbali;

(o) Ushuru wa Vibao vya Matangazo

(p) Ushuru wa Kuchinja, kuwamba na kununua ngozi

Mabadiliko ya viwango vya ada na ushuru

5. Halmashauri itakuwa na Wajibu wa kubadilisha viwango vya Ada na Ushuru pale itakapoona kuwa inafaa kwa kushirikisha wadau, na kutangaza katika Sheria Ndogo hizi kama Marekebisho.

Taratibu za kulipa Ada na Ushuru

6. -(1)Itakuwa ni Wajibu wa kila mtu anayetakiwa kulipa Ada na Ushuru kuhakikisha kwamba analipa Ada na Ushuru kwa viwango vilivyoainishwa kwenye jedwali la Sheria Ndogo hizi.

(2) Muda wa kukusanya Ada na Ushuru utakuwa ni kuanzia Saa Kumi na mbili kamili (12:00) asubuhi mpaka saa kumi na mbili (12:00) jioni.

(3) Bila kuathiri masharti ya kifungu kidogo (2), Maafisa wa Halmashauri au Wakala anaweza kukusanya ushuru baada ya muda uliotajwa hapo juu endapo atakuwa na kibali maalum kutoka kwa Mkurugenzi.

(4) Malipo ya Ada na Ushuru yatafanyika kila siku au kwa mwezi au kwa namna yeyote itakayokubalika kulingana na makubaliano yatakayowekwa kati ya Halmashauri/ Wakala na mlipa ada na ushuru.

(5) Malipo ya Ada na Ushuru yanayotozwa kwa Mujibu wa Sheria Ndogo hizi yatalipwa kwa Halmashauri au Wakala

wake na kutolewa stakabadhi ya Halmshauri kama kielelezo cha malipo yaliyofanyika

Bindhaa za nyumbani

7. Bila kuathiri masharti ya Sheria Ndogo hizi bidhaa zozote zenye uzani usiozidi kilo 50 zitakazoingizwa sokoni na mtu yeyote kwa ajili ya matumzi ya nyumbani hazitatozwa Ushuru au Ada.

Ukusanyaji wa madeni

8. Ikiwa mtu yeyote anayetakiwa kulipa Ada au Ushuru atakataa au kushindwa kulipa Ada au Ushuru ndani ya muda unaotakiwa, Halmashauri inaweza kukusanya Ushuru au Ada unaodaiwa Kwa njia ya Mahakama.

Uteuzi wa Wakala

9. Halmashauri ina Mamlaka ya kumteua Mtu binafsi, Kampuni, Asasi au Taasisi kukusanya Ada na Ushuru kwa niaba yake katika vyanzo vilivyokubaliwa kukusanywa na Wakala.

Wajibu wa Wakala

10. Wakala aliyeteuliwa chini ya Sheria Ndogo hizi atakuwa na wajibu wa-

(a) kukusanya na kupokea Ada na Ushuru katika eneo alilopangiwa kwa kiwango kilichoainishwa chini ya Sheria Ndogo hizi;

(b) kuwasilisha makusanyo yote kwa kuzingatia masharti ya Mkataba wa Uwakala;

(c) kuweka dhamana ya kusanyo la mwezi mmoja kabla ya kuanza makusanyo ambapo dhamana hiyo itarejeshwa mwisho wa Mkataba;

(d) kumchukulia hatua za kisheria mtu yeyote ambaye atakiuka masharti ya Sheria Ndogo hizi;

*Tangazo la Serikali Na. 25 (Linaendelea)*

SEHEMU YA III
MAKOSA NA ADHABU

Makosa

11. (1) Itakuwa ni kosa kwa;

A. Kwa Wakala;

(a) Atakusanya Ada na Ushuru bila kibali cha maandishi au mkataba toka kwa Halmashauri;

(b) Atajaribu au atakusanya ada na ushuru kwa kiwango tofauti na kilichotajwa na Sheria Ndogo hizi;

(c) Atashindwa kuwasilisha au atawasilisha pungufu ya kiwango cha Ada na Ushuru alichokubaliwa katika mkataba;

(d) Atakusanya Ada na Ushuru kwa mbinu tofauti na alizoelekezwa na Halmashauri;

B. Kwa yeyote;

(a) Atashindwa, atadharau, au atakaidi/ Atakataa kulipa Ada na Ushuru au kutekeleza agizo lolote alilopewa na Halmashauri kuhusiana na ulipaji wa Ada na Ushuru chini ya Sheria Ndogo hizi;

(b) Atamshawishi mtu au kundi la watu kukataa au kukwepa kulipa Ada na Ushuru;

(c) Atatengeneza, atatayarisha, ataidhinisha utengenezaji, au atatunza nyaraka za uongo kwa nia ya kujipatia manufaa yatokanayo na ukusanyaji wa Ada na Ushuru mbalimbali ndani ya Halmashauri;

(d) Kwa makusudi huku akijua ni kosa atatoa taarifa za uongo kwa Halmashauri, au Atashindwa au kutoa

*Tangazo la Serikali Na. 25 (Linaendelea)*

taarifa zitakazohitajika na halmashauri;

(e) atashindwa kuweka Kumbukumbu, Vitabu, Hesabu, au maelezo yoyote yatakayohitajika Halmashauri; Na

(f) Atamzuia Afisa Mwidhiniwa au Wakala kutekeleza majukumu yake.

Adhabu

12. Mtu yeyote atakayekwenda kinyume na masharti ya Sheria Ndogo hizi atakuwa ametenda kosa na akipatikana na hatia atatozwa faini isiyozidi shilingi elfu hamsini (Tshs. 50,000/=) au kifungo kisichozidi miezi kumi na mbili (12) au adhabu zote mbili kwa pamoja yaani faini na kifungo.

Kufifilisha kosa

13. Mkurugenzi anaweza kumtoza mtu yeyote faini isiyozidi shilingi elfu hamsini (Tshs.50,000/=) iwapo mkosaji atakiri kosa kwa maandishi na kukubali kutekeleza wajibu wake pamoja na kulipa faini anayodaiwa.

JEDWALI LA KWANZA

(Chini ya kifungu cha 4(1))

1. Ushuru wa Mazao ( Produce Cess Farm gate price)

A. Mazao ya Kilimo

| **Na.** | **Aina ya Mazao** | **Kiwango cha Ushuru (Tshs)** | **Ujazo** |
|---|---|---|---|
| 1. | Mahindi | 1,500/= | kwa debe 6/ kg 100 |
| 2. | Ufuta | 5,000/= | kwa debe 6/ kg 100 |
| 3. | Alizeti /mtama | 2,000/= | kwa debe 6/ kg 100 |
| 4. | Maharage | 1,500/= | kwa debe 6/ kg 100 |
| 5. | Mchele | 5,000/= | kwa debe 6/ kg 100 |
| | | | |
| 6. | Mpunga | 2,000/= | kwa debe 6/ kg |

*Tangazo la Serikali Na. 25 (Linaendelea)*

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | | 100 |
| 7. | Unga wa Muhogo | 3000/= | kwa debe 6/ kg 100 |
| 8. | Mhongo ambao haujatwangwa | 1,000/= | kwa debe 6/ kg100 |
| 9. | Karanga za maganda | 1,500/= | kwa debe 6/ |
| 10. | Karanga zilizomenywa | 5,000/= | kwa debe 6/ kg100 |
| 11. | Mbaazi na jamii zake | 3,000/= | kwa debe 6/ kg100 |
| 12. | Ulezi | 2,000/= | kwa debe 6/ kg100 |
| 13. | Ndizi | 2,000/= | Kwa mkungu |
| 14. | Miwa | 1000/= | Kwa tani moja |
| 15. | Bidhaa nyingine zozote ambazo hazikutajwa | 500/= | |

B. Mazao ya Misitu (Forest Produce Farm gate price)

| Na. | Aina ya Mazao | Kiwango cha Ushuru (Tshs) |
|---|---|---|
| 1. | Mkaa | 1,000/= kwa gunia |
| 2. | Fito | 100/= |
| 3. | Mirunda | 100/= |
| 4. | Asali | 2,000/=kwa lita 20 |
| 5. | Nta | 300/= kwa kilo moja |
| 6. | Kuni tani 7 | 5,000/= |
| 7. | Bidhaa nyingine zozote ambazo hazikutajwa | 500/= |

2. Ushuru wa Mifugo na machinjio ya Mifugo.

A. Ushuru wa Mifugo (Mnadani)

Na. Aina ya Mifugo Kiasi cha Ushuru kwa kila Mfugo (Tshs)

1. Ng’ombe……………………...................................…. 3,000/=
2. Mbuzi…………………………………….........................1,000/=
3. Kondoo……………………………………….…….1,000/=
4. Nguruwe…………………………………….….….1,500/=

*Tangazo la Serikali Na. 25 (Linaendelea)*

B. Ushuru/ ada ya Machinjio na Ukaguzi wa Nyama.

Na.Aina ya Mifugo Ushuru wa Machinjio naAda ya Ukaguzi wa Nyama (Tsh)

1. Ng'ombe………………………………………………… 3,000/= kila mmoja
2. Mbuzi…………………………………………………1,000/= kila mmoja
3. Kondoo……………………………………………..1,000/= kila mmoja
4. Nguruwe…………………………………………....1,500/= kila mmoja.

3. Ushuru wa Soko:

A. Ushuru wa Kushusha Mizigo katika Eneo au Soko lolote liliotengwa na Halmashauri

| *Na.* | Aina ya Mizigo na uzani | Kiwango cha Ushuru (Tshs) |
|---|---|---|
| *1.* | Lori liliobeba Ndizi lenye uzani wa tani 1 | 5,000/= |
| *2.* | Lori lililobeba Miwa, Machungwa, Parachichi nyanya au Nanasi lenye uzani wa tani 1 | 6,000/= |
| *3.* | Mkaa kwa gunia | 1,000/= |
| *4.* | Tenga au gunia la dagaa, Samaki | 1,000/= |
| *5.* | Gunia la Mahindi, Maharage, Kunde | 2,000/= |
| *6.* | Karanga za maganda na mpunga, | 2500 |
| *7.* | Mchele na karanga zilizomenywa | 5,000 kwa gunia |
| *8.* | Tenga la Machungwa, Parachichi, Nanasi, Papai au Nyanya | 500/= kwa tenga |

B. Ushuru wa bidhaa mbalimbali katika masoko, minada, magulio na maeneo mbalimbali yaliyotengwa na Halmashauri :

| Na | Aina ya Biashara | Ushuru/Kodi ya Pango | Muda |
|---|---|---|---|
| 1. | Vibanda | Tshs. 15,000/= kwa kibanda | kwa mwezi |
| 2. | Meza | Tshs. 300/= kwa meza | Kwa siku |
| 3. | Wauza mitumba | Tshs 500/= | Kwa siku |
| 4. | Nguo za madukani kutandaza | Tshs.1,000/ | Kwa siku |
| 5. | Ndizi kupika mkungu | Tshs. 200/= | Kwa siku |
| 7. | Ndizi mbivu mkungu | Tshs. 200/= | Kwa siku |
| 8. | Nanasi tenga | Tshs. 500/= | Kwa siku |
| 9. | Maparachici tenga | Tshs. 500/= | Kwa siku |
| 10. | Mboga-mboga tenga | Tshs. 200/= | Kwa siku |
| 11. | Nyanya/ nyanya mshumaa tenga | Tshs. 300/= | Kwa siku |

*Tangazo la Serikali Na. 25 (Linaendelea)*

| | | | |
|---|---|---|---|
| 12. | Machungwa tenga | Tshs. 200/= | Kwa siku |
| 13. | Viatu vya mitumba | Tshs.1,000/= | Kwa siku |
| 14. | Mama au Baba lishe | Tshs.500/= | Kwa siku |
| 15. | Vyombo vya ndani | Tshs.500/= | Kwa siku |
| 16. | Nyama au nyama choma | Tshs. 1,000/= | Kwa siku |
| 17. | Urembo | Tshs.500/= | Kwa siku |
| 18. | Bidhaa mchanganyiko | Tshs.500/= | Kwa siku |
| 19. | Samani (furniture | Tshs. 5,000 | Kwa mwezi |
| 20. | Wauza vyungu | Tsh 500/= | Kwa siku |
| 21. | Wauza miwa | Tsh 500/= | Kwa siku |
| 22. | Wauza bia na soda | Tsh 1,000/= | Kwa siku |
| 23. | Wauza Pombe za kienyeji | Tsh 500/= | Kwa siku |
| 24. | Wauza madawa ya asili | Tsh 500/= | Kwa siku |
| 25. | Bidhaa nyingine zozote ambazo hazikutajwa | Tshs.500/= | Kwa siku |

4. Ada ya Kibali cha Biashara mbalimbali zisizohitaji leseni.

| | **Aina ya kibali** | **Kiwango cha Ada ya maombi ya kibali (Tshs)** |
|---|---|---|
| 1. | Biashara ya mitumba nje ya maeneo ya magulio, soko na minada | Tshs. 1000/= kwa mwezi |
| **2.** | Fundi cherehani, baiskeli dobi, radio, TV, Fundi simu | Tshs. 1000/= kwa mwezi |
| **3.** | Fundi viatu, | Tshs 500 kwa mwezi |
| 4. | kinyozi, saluni za wanawake/ wanaume | Tshs. 5,000/= kwa mwezi |
| 5. | Mikokoteni, matoroli yenye magurudumu | Tshs. 200/= kwa siku |
| 6. | Kibali cha biashara nyinginezo zisizohitaji leseni | Tshs. 2, 000/=kwa mwaka |

5. Ada ya Kibali cha Ujenzi.

| | | |
|---|---|---|
| 1 | Ujenzi wa Nyumba ya makazi | 30, 000/= |
| 2 | Ujenzi wa Ghala, Karakana, gereji au karakana za magari | 50,000/= |
| 3 | Ujenzi wa Viwanda vidogo vidogo, mashine za kukoboa au kusaga nafaka (mchele, mahindi | 30,000/= |
| 4 | Ujenzi wa Nyumba ya ghorofa moja | 40,000/= |
| 5 | Ujenzi wa Kibanda chochote cha biashara | 6,000/= |

*Tangazo la Serikali Na. 25 (Linaendelea)*

| | | |
|---|---|---|
| | Ujenzi wa uzio wakati wa kujenga jengo lolote | .50, 000/= |

6 . Ada yaukaguzi wa Ramani, Kubadili matumizi ya Majengo *na* Ukaguzi wa Majengo.

| | Aina ya kibali | Kiwango cha Ada ya kibali |
|---|---|---|
| 1 | Kukagua ramani ya jengo la Nyumba ya makazi | Tshs. 10, 000/= |
| **2** | Kukagua ramani ya Ujenzi wa Gorofa kwa kila hatua ya ujenzi. | Tshs. 15,000/= |
| 3 | Kuendelea na hatua ya ujenzi inayoendelea baada ya kibali cha awali | Tshs.5,000/= |
| 4 | Ramani za maghala | Tshs, 15, 000/= |
| 5 | Ramani za Makanisa na misikiti | Tshs. 15, 000/= |

1. Kibali cha idhini ya kubadilisha matumizi ya Ardhi/ viwanja kutoka:-
   i. Makazi kwenda biashara…………....................................Tshs 50,000/=
   ii. Makazi kwenda kwenda viwanda……………………Tshs. 100,000/=
   iii. Biashara Kwenda Makazi………………………………Tshs. 40,000/=
   iv. Biashara/ makazi/ viwanda Kwenda matumizi Mengine Tshs 100,000/=
2. Kibali cha idhini ya kuhamisha miliki ya Ardhi ………………..…Tsh 40,000/=

**7.** Ada ya Kuchangiaji gharama za Upimaji na Usafishaji wa Viwanja

Na. Aina ya Kiwanja Kiwango cha Ada
1. Kiwanja chenye Ujazo wa Msongamano Mkubwa (HD)…..Tshs. 40, 000/=
2. Kiwanja chenye Ujazo wa Msongamano wa Kati (MD)……Tshs. 50, 000/=
3. Kiwanja chenye Ujazo wa Msongamano Mdogo (LD)……..Tshs. 60, 000/=
4. Viwanja vya Taasisi za watu Binafsi/dini……………………Tshs100,000/=
5. Mashamba………………………Tshs. 100, 000/= kwa kila ekari moja.
6. Kurudia upimaji upya baada ya mipaka kufutika 50% ya ada ya upimaji wa kiwanja au eneo husika.
7. Kurudia kuonyeshwa kiwanja baada ya ugao wa awali kufanyika…Tshs.10, 000/=

8. Kodi ya Ardhi kutokana na Makusanyo ya Kodi ya Viwanja kwa mapato ya Serikali Kuu (Land Rent)

Na. Aina ya Kodi Kiwango cha kodi (Tshs)
1. Ushuru utokanao na Uwakala wa Kukusanya Kodi ya Viwanja kwa ajili ya mapato ya Serikali Kuu (Land Rent …30% ya makusanyo halisi.

*Tangazo la Serikali Na. 25 (Linaendelea)*

9. Ada ya Leseni mbalimbali

| **Na.** | **Aina ya Leseni au Kibali** | **Kiwango cha Ada (Tshs)** |
|---|---|---|
| **1.** | Leseni ya pombe za kigeni | Tshs 40,000 kwa miezi Sita |
| **2.** | Leseni ya Pombe za Kienyeji | Tshs 20,000.kwa miezi sita |
| **3.** | Leseni ya Mazao ya Misitu | 20% ya gharama/ ushuru wa leseni |

10. Ada ya zabuni

| **Na.** | **Aina ya Zabuni** | **Kiwango cha Ada (Tshs)** |
|---|---|---|
| 1. | Zabuni ya ujenzi wa majengo, barabara na miundo mbinu mingine | 100, 000/= |
| 2. | Zabuni za uwakala mbalimbali | 50, 000/= |
| 3. | Zabuni za ugavi wa huduma mbalimbali | 50, 000/= |

11. Ada ya Uthamini wa Ardhi na Viwanja vya taasisi binafsi na watu binafsi

| **Na.** | **Aina ya Thamani** | **Kiwango cha Ada (Tshs)** |
|---|---|---|
| 1. | Kiwanja cha Ukubwa wowote | 10 % ya kiwango cha thamani ya kiwanja |
| 2. | Shamba lenye ukubwa wowote | 10% ya kiwango cha thamani ya shamba |

12. Ada ya kibali cha kusafirisha ngozi

| **Na** | **Aina ya Ngozi** | **Kiwango cha Ada (Tshs)** |
|---|---|---|
| 1. | Ngozi za ng'ombe | Tshs. 1,000/= |
| 2. | Ngozi za mbuzi | Tshs. 500/= |
| 3. | Ngozi za Kondoo | Tshs. 500/= |

13. Kodi , Ushuru na Ada ya kukodi vifaa, mali ukumbi na mitambo ya Halmashauri.

| **Na.** | **Aina ya kibali** | **Ada ya Kibali** |
|---|---|---|
| 1. | Mitambo ya Halmashauri lori tani 7 hadi 10 | Tshs 500/= kwa kilometa |
| 2. | Ukumbi wa Mikutano wa Halmashauri ( mdogo) | Tshs150,000/ kwa siku moja |
| 3. | Ukumbi wa Mikutano wa Halmashauri (mkubwa) | Tshs.300,000/ kwa siku moja. |

*Tangazo la Serikali Na. 25 (Linaendelea)*

| | | |
|---|---|---|
| 4. | Vifaa/Mali za Halmashauri kiti au meza za ukumbi wa mkutano wa Halmashauri | Tshs 300@kiti 500/= meza kwa si |
| 5. | Maeneo ya wazi/ barabara kwa ajili ya shughuli za promosheni na matangazo ya biashara | Tshs10,000/ kwa siku |

**14. Faini na Adhabu kwa makosa Mbalimbali (Fines and penalties) ya uzururaji wa mifugo.**

**Na. Aina ya Mifugo/ wanyama kiwango cha Faini au adhabu (Tshs) kwa kosa.**

i. Punda …………………………………………………………….Tshs.5,000/=

ii. Mbwa…………………………………………………………..Tshs. 10,000/=

iii. Ng'ombe……………………………………………………….Tshs. 20,000/=

iv. Nguruwe…………………………………………………… Tshs. 10,000/=

v. Mbuzi…………………………………………………………..Tshs. 10,000/=

**15. Ushuru wa vibao vya matangazo**

| *Na* | *Aina ya Tangazo* | *Ushuru (Tshs) Kwa mwaka* |
|---|---|---|
| 1. | Ada ya Tangazo lenyewe | 2,000/- |
| 2. | Matangazo yanayotoa mwanga | 8,000/- kwa kila mita moja ya mraba |
| 3. | Matangazo yasiyokuwa na mwanga | 6,000/- kwa kila mita moja ya mraba |
| 4. | Matangazo yanayotoa na yasiyotoa mwanga yasiyofika mita moja ya mraba | 4,000/- |

16. USHURU WA KUCHINJA, KUWAMBA NA KUNUNUA NGOZI

| Na. | AINA YA MNYAMA | USHURU WA KUCHINJA | USHURU WA KUWAMBA | USHURU WA KUNUNUA NGOZI |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Ng'ombe | 3,000/= | 1000/= | 1500/= |
| 2. | Mbuzi | 1,000/= | 500/= | 1000/= |
| 3. | Kondoo | 1,000/= | 500/= | 1000/= |
| 4. | Nguruwe | 1,500/= | 500/= | 1,000/= |
| 5. | Mnyama mwingine | 1,000/= | 500/= | 1000/= |

*Tangazo la Serikali Na. 25 (Linaendelea)*

JEDWALI LA PILI

HATI YA KUKIRI NA KUFIFILISHA KOSA

*(Chini ya kifungu cha 13)*

Mimi …………………… nakiri mbele ya ………….ambaye ni Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashuri ya Wilaya ya Mlele, kwamba mnamo tarehe …… ya Mwezi ……. Mwaka …… nilitenda kosa la kukiuka masharti ya kifungu cha …… cha Sheria Ndogo za (Ada na Ushuru) za Halmashauri ya Wilaya ya Mlele za Mwaka 2016.

Kwa Mamlaka aliyopewa Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri, Niko tayari kulipa kiasi cha Ada/ Ushuru ninaodaiwa pamoja na faini.

NATHIBITISHA KWAMBA MAELEZO HAPO JUU NI YA KWELI NA NIMEYATOA KWA HIARI YANGU KADRI YA UFAHAMU WANGU

Leo tarehe…………. ya Mwezi………… Mwaka ………………….
*Jina.……………………………..* *Saini.…………………………..*

Mbele ya :

Jina: ……………………………………………
Cheo: ………………………………………….
Saini: …………………………………………..

Nembo ya Halmashauri ya Wilaya ya Mlele imebandikwa katika Sheria hizi Ndogo kutokana na Azimio la kikao cha Halmashauri ya Wilaya ya Mlele kilichoketi tarehe 17 mwezi 07 mwaka 2015 na lakiri imebandikwa mbele ya:-

GODWIN L. BENNE,
*Mkurugenzi Mtendaji*
*Halmashauri ya Wilaya ya Mlele.*

DUES J. BUNDALA,
*Mwenyekiti*
*Halmashauri ya Wilaya ya Mlele.*

NAKUBALI,

Dodoma,
09 Januari, 2017

GEORGE B. SIMBACHAWENE (MB)
*Waziri wanchi-or-Tamisemi.*

*Tangazo la Serikali Na. 25 (Linaendelea)*